



Na.20: Msimu wa Kilimo 2025/26

Tathmini ya Aprili 11-20, 2026 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 21-30, 2026

### MUHTASARI

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo machache ya nchi zitasaidia kuimarisha unyevu wa udongo, hivyo kusaidia katika ukuaji wa mazao na upatikanaji wa malisho.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika mikoa ya Dodoma na Singida inatarajiwa kusaidia maendeleo ya mazao hususan zao la alizeti lilipo katika hatua ya kutoa maua na kukomaa
- Wakulima na wadau wa kilimo wanashauriwa kushirikiana na maafisa ugani katika maeneo yao, sambamba na kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2026


**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kupungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuendelea kuwepo katika maeneo mengi ya nchi na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo. Aidha, upepo wa bahari wenye unyevunyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani uliimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na ukanda wa pwani; na vipindi vya mvua katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, nyanda za juu kusini magharibi na kanda ya kusini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa viliripotiwa katika maeneo ya ukanda wa pwani, na ukanda wa Ziwa Victoria.

### TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2026

**K**atika dekadi hii, maeneo mengi ya nchi yalipata kiasi cha mvua za siku kumi kati ya milimita 10 hadi 200, hali inayoashiria usambazaji mzuri wa mvua katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya Dodoma na Singida yalikuwa makavu kwa ujumla.

Kiasi kikubwa zaidi cha mvua zaidi ya milimita 200 kilirekodiwa katika maeneo machache ya mikoa ya Njombe, Ruvuma na Tanga kama inavyooneshwa katika Kielelezo cha 1.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 11-20, 2026

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2026

**K**atika dekadi hii, maeneo mengi nchini yalipata mvua ambayo ilisaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo, kutuama kwa maji katika maeneo ya mabondeni, hususan katika maeneo machache ya mikoa ya ukanda wa pwani.

Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan ukanda wa pwani ya kaskazini, bonde la Ziwa Victoria na sehemu za nyanda za juu kaskazini mashariki, mahindi yapo katika hatua ya kubumba na kutoa mbelewele na wakulima waliendelea na shughuli za usimamizi wa mashamba kama vile upulizaji dawa za kuuwa wadudu waharibifu.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kuchanua hususan katika mkoa wa Morogoro na katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Rukwa, Mwanza na Mbeya. Katika mikoa ya Morogoro na Dodoma zo la alizeti lipo katika hatua ya kutoa maua.

Kwa upande wa mazao ya kudumu, zao la kahawa katika mikoa ya Kilimanjaro na Songwe lilikuwa katika hatua ya kuiva kwa matunda wakati zao la karafuu likiwa kwenye hatua ya makonyo katika kisiwa cha Pemba. Kiwango kizuri cha unyevunyevu wa udongo katika kipindi hiki kimekuwa muhimu kwa ukuaji wa matunda, na wakulima waliendelea na shughuli za usimamizi wa mazao

Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yapo katika hatua za awali za kukomaa wakati katika mkoa wa Tabora mahindi yalikuwa katika hatua za mwisho za kukomaa na kukauka na baadhi ya wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa zao hilo.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori uliendelea kuimarika katika maeneo yaliyopata mvua za kutosha.

### HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2026

**K**wa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kiliongezeka kidogo hususan kwa maeneo ambayo yalipata mvua.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo.

Aidha, upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani unatarajiwa kuendelea kuimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**M**aeneo ya kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), pwani ya kaskazini (Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi), kanda ya kusini (Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) kunatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) kunatarajiwa kupata vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache hususan ya mkoa wa Kigoma.

Kanda ya kati (Dodoma na Singida) kunatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) kunatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

### HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**H**ali ya mvua inayotarajiwa katika maeneo machache nchini itaendelea kusaidia kuongeza unyevu nyevu katika udongo na kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika mikoa ya Dodoma na Singida inatarajiwa kusaidia maendeleo ya mazao hususan zao la alizeti lilipo katika hatua ya kutoa maua na kukomaa.

#### Ushauri:

- **Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (kanda ya Ziwa Victoria, Pwani ya Kaskazini na Nyanda za juu Kaskazini Mashariki):** Wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kuchukua tahadhiri kutokana na uwepo wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na kupulizia dawa mara tu itakapohitajika. Pia wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku kwa mipango thabiti ya shughuli za kilimo.
- **Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua (Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Mikoa ya Magharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya Kati na Kusini):** Wakulima wanashauriwa kufuatilia hali ya mazao na pia kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku.
- **Malisho na upatikanaji wa maji kwa wafugaji:** Wafugaji wanashauriwa kuendelea kupanda majani ya malisho na kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- **Wavuvi wa Samaki baharini na maziwa makuu:** Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kujua wakati sahihi wa kufanya shughuli za uvuvi kutokana na uwezekano wa kujitokeza mawimbi makubwa na upepo mkali

Ushauri huu umedhamiria kuongeza tija kwenye kilimo na kupunguza athari zitokanazo na hali mbaya ya Hewa. Wadau wote wa kilimo wanahimizwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa ili kuwa na mipango thabiti ya shughuli za kilimo.

### HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2026

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kubaki kawaida katika maeneo mengi. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.